

MKATABA WA UPANGISHAJI CHUMBA CHA **BIASHARA**

MAKUBALIANO HAYA YAMEFANYIKA _____
BAINA YA
MPANGISHAJI _____
NA
MPANGAJI _____

Mimi nitaendelea kuwa mmiliki halali wa chumba cha biashara kilichopo
Nyumba namba _____
iliyopo _____ chumba
ambacho ndani ya mkataba huu kinatajwa kama chumba cha biashara basi
mpangaji atatakiwa kuzingatia na kufuata kanuni na masharti yaliyoainishwa
kwenye mkataba huu, ya kumpangisha chumba hiki cha biashara kwa ajili ya
kufanyia biashara yake halali.

MAKUBALIANO:

1. **MPANGAJI** atatakiwa kufanya malipo ya **KODI** yaliyoainishwa
katika mkataba huu, na kulingana na masharti ya upangaji kama
yanavyoainishwa kwenye mkataba huu
2. **MPANGAJI** atalipa TZS _____ kwa mkupuo ikiwa ni malipo
ambayo ni kodi ya miezi sita kwa kiwango cha TZS _____
kwa mwezi;
3. **MPANGAJI** atalazimika kuwa mlinzi wa mali zake bila kumhusisha
mpangishaji
4. **MPANGAJI** atatakiwa kugharamikia huduma ya nishati ya umeme
na huduma ya maji kulingana na kanuni au maelewano
watakayojiwekea yeye pamoja na wapangaji wenzake
5. Mkataba huu umeanza kutumika tarehe _____

MASHARTI YA UPANGAJI:

- a) Endapo
 - I. Katika kipindi cha upangaji kodi haitokua imelipwa kwa muda wa
siku kumi au
 - II. **MPANGAJI**, bila sababu ya msingi, akashindwa kuzingatia
masharti muhimu ya upangishaji, katika mkataba huu itakua ni
halali kwangu kutwaa chumba hiki cha biashara;
- b) Pia taarifa (**NOTICE**) inayohusiana na upangaji katika mkataba huu
itakua ni kwa njia ya maandishi;

- c) Mkataba huu unaweza ukarefushwa kulingana na makubaliano yetu pia katika kipindi chote cha kupitia upya na kurefushwa kwake, kiasi cha kodi kitajadiliwa upya kulingana na mazingira ya kibiashara kwa wakati huo
- d) **MPANGAJI** anaweza akavunja mkataba kabla ya kumalizika kwa kipindi chake, baada ya kutoa taarifa kwa **MPANGISHAJI**: lakini kwa hali yoyote, uvunjaji wa mkataba ndani ya kifungu hiki hautoruhusu kurudishwa kwa kodi itakayokua imeshalipwa.

MPANGAJI ANATAKIWA KUFUATA MASHARTI YAFUATAYO:

1. Kulipa **KODI** kwa kwa kiasi kilichotajwa katika mkataba huu;
2. Kulipa Gharama za umeme kwa mamlaka husika;
3. Kwa wakati wote, kuweka chumba cha biashara katika hali bora, na usafi kwa matumizi ya biashara;
4. Kuruhusu **MPANGISHAJI** au mtu yeyote kwa niaba yake, kuingia na kufanya matengenezo au ukaguzi unaohusiana na ubora wa chumba cha biashara;
5. Kutofanya upanuzi, au kubadilisha sehemu yoyote ya chumba cha biashara bila ridhaa ya **MPANGISHAJI**;
6. Kutompingisha mtu yoyote bila ridhaa ya **MPANGISHAJI**;
7. kutotumia chumba cha biashara kwa hali yoyote ambayo itasababisha kero au usumbufu kwa majirani au wafanyabiashara wengine;
8. Kutumia chumba cha biashara kwa madhumuni ya biashara tu;
9. Kwamba Biashara itakayofanyika isiwe ni kinyume cha sheria za nchi;
10. Pia **MPANGAJI** atawajibika kwa uharibifu wa makusudi au uzembe, katika chumba cha biashara;
11. Wakati mkataba utakapofikia ukingoni, na kabla ya kurefushwa kwake, **MPANGAJI** atakabidhi chumba cha biashara kikiwa katika hali nzuri ya kibiashara.

Mkataba huu umesainiwa na

MPANGISHAJI _____

NA

MPANGAJI _____